KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 23, Issue 1

11th Rajab 1433

1st JUNE, 2012

YANAYOHUSIANA NA MWEZI WA RAJAB

NA: QSSEA

Rajab ni miongoni mwa hiyo miezi Mitukufu, iliyochaguliwa na kupewa fadhla maalum. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى) katika Surat at-Tawbah (9)36: **“Idadi ya miezi (ya mwaka mmoja) mbele ya Allaah ni miezi kumi na mbili katika ilimu ya Allaah (Mwenyewe tangu) siku alipoumba Mbingu na Ardhi. Katika hiyo imo minne iliyo Mitukufu kabisa** (Dhul-Qa’dah, Dhul-Hijjah, Muharram na Rajab). **(Kufanya) hivi ndiyo dini iliyo sawa. Basi msijidhulumu nafsi zenu (kwa kufanya ma’asi) katika (miezi) hiyo.”**

Allah ametuamrisha sisi tuzingatie kwa uangalifu kuhusiana na nUtakatifu wa miezi mine hii na tujiepushe na kufanya madhambi ndani yake.

Allaah amesema katika Qur'aan: **"Enyi Mlioamini! Msivunje heshima ya alama za (dini ya) Allaah wala (heshima) ya mwezi uliotukuzwa.”** [Soorah al-Ma'idah (5):2] Kwa maana yakwamba jiepusheni na kufanya madhambi na musivunje sheriya za Allaah, kwani munalazimika kuheshimu na kuitukuza miezi mitakatifu - Makatazo haya yanahusu yote mawili, vitendo vya haramu na imani potofu. Juu ya byote hayo, tunakuta mambo mengi ya uzushi yamezagaa miongoni mwa watu wengi yenye kuhusiana na mwezi wa Rajab, baadhi yao hufunga kwa wingi katika mwezi wa Rajab wakiamini yakwamba kufunga katika mwezi huu kuna malipo makubwa. Kwa vile ni mmojawapo wa miezi Mitukufu, hata kama hakuna dalili iliyo swaheeh yenye kuunga mkono jambo hilo. Kufunga swaum kumependekezwa katika mwezi wa Rajab kama ilivyopendekezwa katika miezi mengine, hakuna hadeeth swaheeh yenye kueleza fadhla maalum au malipo makubwa ya kufunga katika mwezi wa Rajab. Uzushi mwengine ulio maarufu mno wenye kufanywa katika mwezi wa Rajab ni swalaat ur-Raghaa’ib, ambayo ni swala inayoswaliwa katika usiku wa kwanza wa mwezi wa Rajab. Baadhi ya warongo wameizua hadeeth hii katika Qarne ya Nne Kabla ya Hijrah. Hadeeth wanayoitumia katika kutoa hoja ya kuiunga mkono ni ya uzushi kulingana na muafaka wa wanavyuoni wa hadeeth. Vilevile inadaiwa yakwamba Safari Ya Usiku ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) (Isra wal-Miraaj) ilitokea katika tarehe Ishirini na Saba ya mwezi wa Rajab na kwahivyo kisa cha Mi’raaj husomwa, na kusherehekewa katika tarehe ya Ishirini na Saba ya Rajab. Vilevile baadhi ya watu huutenga usiku huo kwa ajili ya kuzidisha kutekeleza vitendo vya ’Ibaadah. Vitendo vyote hivyo havina msingi wowote, kwa sababu hakuna dalili yakwamba “Israa’ wal-Miraaj yenyewe ilitokea tarehe ishirini na saba ya Rajab. Hata kama lau ingelithubutu, basi kulisherehekea tukio kama hilo inakuwa ni uzushi kwani hakuna kitu kama hicho kilichopokewa kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) au Maswahaba zake.

Haya ndiyo mambo machache ya uzushi wa kawaida uliozoeleka inayofanyika katika mwezi wa Rajab, lakini hatahivyo, kuna idadi ya mengine yakiwemo, kuzuru makaburi

'ILMU YENYE MANUFAA

"THE QUR'AN & SUNNAH SOCIETY OF EAST AFRICA" [QSSEA] WANAWAALIKA MIHADHARA YA KI-'ILIMU KATIKA MASJID MAZRUI KUANZIA TAREHE 31st MAY – 3rd JUNE, 2012 [SIKU NNE]

WAKATI WA MIHADHARA:

KUANZIA BA'DAL ASR MPAKA ISHAA'. 4:15pm - 'ISHAA'

MADDA ZITAKAZO ZUNGUMZWA:

- *ATHARI ZA MADAWA YA KULEVYA.
- *MAMBO YENYE KUHARIBU IMANI YA MTU.
- *ADABU ZA MA-SALAF ZILIVYOKUWA.
- *HUKMU ZA SIHRI (UCHAWI) KATIKA UISLAMU.
- *ATHARI ZA TALAKA KATIKA MUJTAMA'
- *MALEZI BORA KATIKA UISLAMU.

YALIYOMO

TANGAZO LA DARSA	1
MWEZI WA RAJAB	1
DU'A' NA KUFUTA USO	2
MAANA YA BID'AH	4 - 3
FATAWA	4

(Endelea Kutoka Uk. 1)

hususan katika mwezi wa Rajab, kusoma Du'aa' maalum katika mwezi wa Rajab, kutekeleza 'Umrah kila ifikapo mwezi wa Rajab, na kadhaalika. Twamuomba Allaah atulinde na kila aina ya uzushi, na atuja'aliye kuwa ni miongoni mwa wenye kuifuata Sunnah ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kisawasawa, na kuviheshimu vile vitu alivyovitukuza Allaah kulingana na alivyopanga Yeye mwenyewe. Aameen.

JEE YAFAA KUOMBA DU'AA' KWA KUINUA MIKONO YAKO KISHA UJIPANGUSIE NAYO USO WAKO ?"

NA : SHEIKH MUHAMMAD NAASIR UD-DEEN AL-ALBAANI

KUTOKA KATIKA: IRWAA' AL-GHALEEL (2/178-182) CHA SHEIKH AL-ALBAANI:

Alipokuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) Akiinua Mikono Yake Anapo Omba dua', Hayashukishi Chini Mpaka Apangusie Nayo Uso Wake."

Dha'eef (Nyonge). Imepokewa na Tirmidhee (2/244) na Ibn 'Asaakir (7/12/2) kupitia kwa: Hammaad Ibn 'Isa al-Juhani kutoka kwa Handhwalah ibn Abi Sufyaan al-Jamhi kutoka kwa Saalim Ibn 'Abdullaah kutoka kwa babake kutoka kwa 'Umar ibn al-Khattaab, aliyesema: ...

Tirmidhee akasema baada yake, "Hii ni hadeeth swaheeh ghareeb. Sisi twaijua tu kama ni hadeeth ya Hammaad Ibn 'Isa, kwani yeye alikuwa peke yake katika kuisimulia; yeye ana ahaadeeth chache tu, lakini watu wamepokea kutoka kwake."

Hatahivyo, mpokezi huyu ni dha'eef, kama ilivyo katika Taqreeb cha Ibn Hajar, aliyemzungumza katika Tahdheeb:

Amesema Ibn Ma'een, "Sheikh mzuri"; Abu Haatim akasema, "Dha'eef katika hadeeth"; Abu Daawud akasema, "Dha'eef, hupokea munkar ahaadeeth"; Haakim na Naqqaash wakasema, "Hupokea ahaadeeth za kuzuliwa kutoka kwa Ibn Juraij na Ja'far as-Saadiq." Amethibitishwa kuwa dha'eef na Daaraqutnee'. Amesema Ibn Hibbaan, "Hupokea vitu ambavyo ni 'kinyume cha ilivyo kutoka kwa Ibn Juraij na 'Abdul 'Azeez Ibn 'Umar Ibn 'Abdul 'Azeez, kiasi cha kwamba ionekane na walio na ujuzi katika ta'aluma hii yakwamba alikusudia; hairuhusiwi kumtumia yeye kama ushahidi." Ibn Maakoolaa amesema, "Wamethibitisha ahaadeeth zake kuwa ni dha'eef."

Kwa hiyo, mfano wa wapokezi kama huyu ni dha'eef mno, kwa hivyo ahaadeeth zake haziwezi kuinuliwa kwenye daraja ya hasan, licha ya swaheeh!

Hadeeth mfano wa hiyo ni:

"Alipokuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akiomba du'a na kuinua mikono yake, alikuwa akifuta uso wake kwa mikono yake."

Dha'eef (Nyonge). Abu Daawud (1492) kutoka kwa Ibn Lahee'ah kutoka kwa Hafs Ibn Hishaam Ibn 'Utbah Ibn Abi Waqqaas kutoka kwa Saa'ib Ibn Yazeed kutoka kwa babake.

Hii ni sanad dha'eef kutokana na Hafs Ibn Hishaam yakwamba ni mtu asojulikana na udhaifu wa huyu Ibn Lahee'ah (cf. Taqreeb at-Tahdheeb). Hadeeth hii haiwezi kutiwa nguvu kwa njia mbili za riwaya kwa pamoja kutokana na uzito wa udhaifu wa hadeeth ya kwanza, ambao ushauona.

Dha'eef (Nyonge): Imepokewa na Ibn Maajah (1181, 3866), Ibn Nasr katika Qiyaam al-Lail (Uk. 137), Tabaraani katika Al-Mu'jam al-Kabeer (3/98/1) na Haakim (1/536), kutoka kwa Saalih Ibn Hassaan kutoka kwa Muhammad Ibn Ka'b kwa njia ya marfoo' kutoka kwa Ibn 'Abbaas (رضي الله عنه)

Hii ni sanad dhaifu mno kutokana na Ibn Hassaan, ambaye ni munkar katika Hadeeth, kama alivyosema Bukhaari; Nasaa'ee akasema, "Huyu ametupiliwa mbali katika Hadeeth"; Ibn Hibbaan amesema, "Alikuwa na waimbaji wanawake na yeye mwenyewe alikuwa akisikiza nyimbo, na alikuwa akisimulia khabari za kuzua kutoka kwa wapokezi waaminifu"; Ibn Abi Haatim amesema katika Kitaab al-'Ilal (2/351), "Nilimuuliza babangu (Yaani: Abu Haatim ar-Raazi) kuihusu hadeeth hii, ambayo aliyoisema kuwa ni: 'Munkar'." Ibn Hassaan ameungwa mkono na 'Isa Ibn Maimoon, ambaye pia aliyeipokea kutoka kwa Muhammad Ibn Ka'b, kama ilivyopokewa na Ibn Nasr. Lakini hata hivyo, hii haibadilishi chochote, kwa vile Maimoon mwenyewe pia ni dha'eef: Ibn Hibbaan akasema, "Anapokea ahaadeeth, ambazo zote ni za kuzua"; Nasaa'ee akasema, "Si muaminifu."

Hadeeth hii ya Ibn 'Abbaas pia imepokewa na Abu Daawud (1485), na Baihaqee kutoka kwake (2/212), kwa kupitia kwa: 'Abdul Maalik Ibn Muhammad Ibn Aiman kutoka kwa 'Abdullaah Ibn Ya'qoob Ibn Is-haaq kutoka kwa mtu aliyemsimulia yeye kutoka kwa Muhammad Ibn Ka'b, maneno yasemayo:

"Musizizibe kuta. Mwenye kusoma barua ya ndugu yake bila ya ruhusa yake, kwa hakika anautazama moto. Muombeni Allaah kwa viganja vyenu vya mikono, na wala musimuombe kwa migongo yake, na mumalizapo, ipanguseni kwayo nyuso zenu."

Hii ni sanad dhaifu: 'Abdul Maalik amethibitishwa kuwa dhaifu na Abu Daawud; vilevile ndani yake yumo Sheikh wa 'Abdullaah Ibn Ya'qoob ambaye jina lake hakutajwa, na kwahivyo, amebakia kuwa ni mtu asojulikana – pana uwezekano kuwa huwenda akawa ndiye huyo Ibn Hassaan au Ibn Maimoon, wote wakiwa ni miongoni mwa waliotajwa hapo juu.

Hadeeth hiyo vilevile imepokewa na Ibn Haakim (4/270) kwa njia ya: Muhammad Ibn Mu'aawiyah, aliyesema yakwamba Masaadif Ibn Ziyaad al-Madeeni alimsimulia yakwamba aliisikiya kutoka kwa Muhammad Ibn Ka'b al-Qurazi. Adh -Dhahabi akaifuatilia kwa kutaja yakwamba Ibn Mu'aawiyah amethibitishwa kuwa ni mrongo na Daaraqutnee', kwahivyo hadeeth hiyo imeorodheshwa miongoni mwa hadeeth za urongo.

Abu Daawud amesema kuihusu hadeeth hii, "Hadeeth hii imepokewa kwa kupitia njia zaidi ya moja kutoka kwa Muhammad Ibn Ka'b; wote hao ni dhaifu."

Kunyanyua mikono katika Qunoot kwa ajili ya janga fulani imethubutu kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipowaapiza washirikina waliowauwa mahuffaadh (waliohifadhi Qur'an) sabiini – Imepokewa na Imaam Ahmad (3/137) na Tabaraani katika al-Mu'jam as-Sagheer (Uk. 111) kama ilivyo katika hadeeth ya Anas kwa sanad iliyo swaheeh. Imethubutu mfano wake kutoka kwa 'Umar na wengineo katika Qunoot ya Swala ya Witr. Hatahivyo, kwa vile kujipangusa uso (au kufuta uso)

(Endelea Uk. 3)

(Endelea Kutoka Uk. 2)

baada ya du'a al-Qunoot haikuwahi kupokewa kabisa kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) wala kutoka kwa Swahaba wake yoyote, linakuwa hilo ni jambo la kuzua bila ya shaka yoyote.
Ama kuhusu kupangusa uso baada ya du'a nje ya swala, kuna ahaadeeth hizo mbili pake yake; si sawa kusema yakwamba ahaadeeth hizo zinasaidiana kutia nguvu ili zifikie daraja ya Hasan, kama alivyofanya Manaawi, kutokana na udhaifu wake wa kupindukia uliopatikana katika njia za mapokezi. Hii ndiyo sababu Imaam an-Nawawi akasema katika al-Majmoo' , "Haijuzu" (yaani: Haifai kufuta uso), akathibitisha Ibn 'Abd as-Salaam, aliyesema, "Mtu mjinga peke yake ndiye mwenye kufanya hivyo."
Rai yakwamba kupangusa uso baada ya du'a haikuthubutu imetiliwa nguvu na ukweli yakwamba kuna ahaadeeth nyingi sana zilizo swaheeh zinazohusu kuinua mikono katika du'a, na hakuna hata mojawapo inayotaja kuhusu kupangusa uso, hii yaonyesha yakwamba, Insha-Allaah, ni jambo lisilofaa na halikuthubutu.

MAANA YA BID'AH NA UBAYA WAKE!

Ki-Lugha, maana ya Bid'ah (uzushi) ni 'jambo jipya lililozushwa'. Maana ya ki-Sheriya ya Bid'ah ni: "Njia mpya iliyozushwa [ya Imani au vitendo] katika Dini, iliyokusudiwa kuiga Sheriya, ambayo malengo yake ni kujikurubisha kwa Allaah, [lakini ikawa] haina usaidizi wa dalili yoyote iliyo swaheeh - si katika misingi yake, wala si katika njia inayotumika kufanya." Al-I'tiswaam of ash-Shaatibee (1/37).

Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Kila jambo la uzushi ni upotofu."* Imepokewa na Abu Daawud (no. 4607), at-Tirmidhee (no. 2676) na ni swaheeh. Ibn Hajar ameiswahihisha katika Takhreej Ahaadeeth Ibn ul-Haajib (1/137).

Na akasema tena (صلى الله عليه وسلم): *"...Kila jambo la uzushi ni upotofu na kila upotofu, huishia motoni."* Imepokewa na an-Nasaa'ee (1/224) kutoka kwa Jaabir bin Abdullaah na ni swaheeh kama ilivyobainishwa na Shaikh ul-Islaam Ibn Taymiyyah katika Majmoo' ul-Fataawaa (3/58).

Vilevile Mtume (صلى الله عليه وسلم) ametoa makemeo makali dhidi ya wazushi, katika kushikana na kufanya urafiki nao, kuwasaidia au kuchukuwa kutoka kwao aliposema: *"Yoyote atakaezua jambo au atakaemsaidia mzushi, basi juu yake ni la'ana ya Allaah, na Malaika wake, na watu wote."* Imepokewa na al-Bukhaaree (12/41) na Muslim (9/140)

Na katika mafunzo yao, tunawaona Maswahaba watukufu na ma-Taabi'een waliokujan baada yao wakionya kutokamana na hatari za uzushi juu ya Ummah, watu wake na Umoja wao, kwani ni mambo ya uzushi ndiyo yaliyougawanya Ummah na kuufarakanisha.

Ibn Abbaas (k. 68H) amesema: "Kwa hakika, jambo lichukizalo mno mbele ya Allaah ni Uzushi." Imepokewa na al-Bayhaqee katika as-Sunan al-Kubraa (4/316)

Ibn Umar (f. 84H) amesema: "Kila jambo la uzushi ni Upotofu, hata kama watu wataliona kuwa ni jambo zuri." Imepokewa na Abu Shaamah (no. 39)

Siku moja Ahmad Ibn Hanbal alisema, "Mtenda dhambi mkubwa (faasiq) miongoni mwa Ahl-Sunnah Wal Jamaah ni bora kuliko mtu mwema mno miongoni mwa Ahl-"Bid'ah".

Amesema 'Abdullaah ibn Mas'ood, "Fuata na wala usizue, kwani umepewa yenye kukutosheleza na kila jambo la uzushi ni upotofu." Imepokewa na Abu Khaithamah katika 'Kitaab Ul-'Ilm' (no. 540) na kuswahihishwa na Shaikh al-Albaanee.

Amesema 'Abdullah Ibn Abbaass, "Pindi inapozuliwa Bid'ah, basi Sunnah hufa na hili huendelea hivyo mpaka Bid'ah hiyo ikawa inaishi na Sunnah ikawa imekufa." Al-'Irbaad ibn Saariyah, , amepokea yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Mimi nimewawacha nyinyi juu ya uongofu ulio wazi kabisa. Usiku wake ni kama mchana wake. Hapana yoyote apotokae kutoka katika njia hiyo [baada ya kuondoka kwangu], isipokuwa huwa ameangamia."* Imepokewa na Ahmad, Ibn Maajah (no. 43) na al-Haakim. Imeswahihishwa na Shaikh al-Albaanee katika as-Saheehah (no. 937).

Amepokea Al-Marwazee katika as-Sunnah (no. 95) yakwamba 'Umar ibn 'Abd Allah-'Azeez amesema, "Hapana udhuru kwa yoyote, baada ya Sunnah, kupotea katika makosa aliyodhania kuwa ni Uongofu."

Hasan Ibn Attiya, mmojawapo miongoni mwa Taabi'een amesema, "Watu wanapoikubali "Bid'ah", Allaah huiondoa Sunnah miongoni mwao na wala hairudishi kwao mpaka siku ya Malipo."

Mmojawapo wa wanavyuoni wa zamani, Al-Barbahaaree, aliye miongoni mwa marafiki wa Ahmad Ibn Hanbal, amesema, "Jitahadhari na "Bid'ah", kwa sababu kila "Bid'ah" ilianza kama jambo dogo lenye kufanana na ukweli, mara watu wakahadaika nalo wakaanza kulifuata mpaka likawa kubwa na kuzidi kuwa kubwa wakanaswa nalo na kuwatoa nje ya Uislamu."

Vilevile Shaykh al-Barbaharee (k. 329H رحمه الله) alisema: Rehma za Allaah zikushukie wewe. Jua yakwamba Dini ni ile iliyokuja kutoka kwa Allaah (سبحانه وتعالى) na si jambo lililoachiwa akili na rai ya mtu kujichagulia. 'Ilmu yake ni ile itokayo kwa Allaah na Mtume wake, kwahiyo usifuate chochote kilichotegemea mapedelewa ya nafsi yako, ukapotoka na kutoka katika Dini ukauwacha Uislamu. Hutokuwa na udhuru, kwani Mtume (صلى الله عليه وسلم) ameifundisha Sunnah kwa Ummah wake mzima na kuibainisha kwa Maswahaba zake, nao ndiwo Jamaa'ah nao ndiwo Mwili Mzima, na mwili mzima ndiyo Haki na wafuasi wake.

Mas'ala haya vilevile yameashiriwa na Imaam Maalik (رحمه الله) katika athari yake moja inayostahiki kuandikwa kwa wino wa dhahabu. Nao ni msemo wake aliposema: "Yoyote atakaezua jambo katika Uislamu, ambalo atakalochukulia kuwa ni zuri, basi atakuwa amedai yakwamba Muhammad amewahadaa Waislamu (uaminifu wa ulinganizi) ujumbe wake. Soma maneno ya Allaah (سبحانه وتعالى): **"Leo hii i**n**imewakamilishia Dini yenu, na nimewatimizia ne'ma Zangu juu yenu, na nimeiridhia Dini ya Uislamu kuwa ndiyo Dini yenu.'** [Surat-ul-Maa'idah: 3].

Kwahiyo lolote ambalo halikuwa [ni katika sehemu] ya Dini wakati huo, halitokuwa [ni katika sehemu] ya Dini siku hii ya leo. Na sehemu ya mwisho ya Ummah huu halitorekebishika, isipokuwa kwa kile kilichourekebisha sehemu yake ya mwanzo." Ibn Taymiyyah ana insha nzuri sana katika mojawapo ya vitabu vyake inayo onyesha yakwamba: "Kwa hakika, ukafiri wa Mayahudi na Manaswara umetokana na "Bid'ah". Walizua

mambo mapya kwenye Dini na mambo hayo yakawatoa kabisa mbali na ujumbe wa Musa na 'Isaa (عليهما السلام)." Kwahiyo, kama ambavyo hali za Wa-arabu katika zama za ujinga hazikurekebishika isipokuwa kwa kuja kwa Mtume wao Muhammad na wahyi kutoka Mbinguni - uliowasaidia katika ulimwengu huu na utakaowasaidia katika ulimwengu ujao - basi msingi haswa yakwamba ubora wa Uislamu ni lazima uimarishwe katika zama hizi, na si chochote , bali ni kurudi kwa Qur'an na Sunnah. Licha ya haya yote, suala hili linahitaji kiasi fulani cha ziyada katika kufahamishana, kutokana na idadi kubwa ya makundi na vyama vya ki-Islamu vilivyoko kwenye majukwaa, na vyenye kujidai yakwamba wao wanafuata njia ambayo Jamii ya ki-Islamu na utawala wa ki-Islamu inaweza kutimizwa ukweli wake.

WAULIZE WANAVYUONI

MWANAMKE HANAJISIKI KWA AJILI YA HEIDH AU KUTOKWA NA DAMU YA MAZAZI

SUALI: Mke wangu amejifungua (amezaa) na mmojawapo wa marafiki zangu akanizuiya nisiingie hapo nyumbani kwangu, kwa madai yakwamba ati hairuhusiwi kwa mtu kula chakula chochote kilichotayarishwa na mwanamke atokwae na damu ya mazazi. Huzingatiwa hali ya mwanamke huyu kuwa amenajisika kimwili na kimaumbile. Natumai utanisaidia katika mas'ala haya. Kulingana na nijuavyo mimi, wanawake wenye kutokwa na damu ya mazazi hawaruhusiwi kuswali, kufunga au kusoma Qur'aan?

JAWABU: Mwanamke hanajisiki kwa ajili ya heidh wala kutokwa na damu ya mazazi. Hakatazwi mtu kula nae wala kugusana nae kimwili, maadamu sehemu yake ya tupu itaepukwa. Hatahivyo, ni makuruhu kugusana na sehemu za baina ya kitovu na magoti peke yake. Hii ime-egemezwa juu ya aliyoyapokea Muslim kutoka kwa Anas (**رضي الله عنـه**): Miongoni mwa Mayahudi, pindi mwanamke akiwa katika heidh, huwa hawali chakula na yeye. Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Fanyeni nao kila kitu (mupendavyo, kama kawaida yenu), isipokuwa musijamiiane nao."*

Al-Bukhaari na Muslim pia walinukuu kutoka kwa 'Aa'ishah (رضي الله عنهما) aliyesema yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akimwambia ajifunge kitambara cha kiuno na kisha alikuwa akiamiliana nae kimwili haliyakuwa yuko katika heidh. Hakuna athari yoyote juu ya kula nae au kula chakula alichokitayarisha, kutokamana na kuharamishwa kwa swala, kufunga na kusoma Qur'aan akiwa kwenye heidh na kupata damu ya mazazi.

Kamati ya Wanavyuoni.

KUTUMIA TEMBE ZENYE KUZUIYA HEIDH:

SUALI: Kuna tembe zenye kuzuiya heidh au kuichelewesha kutokea. Jee, mwanamke anaruhusiwa kutumia tembe kama hizo katika wakati wa Hijjah kwa kuchelea heidh yake isimjie?

JAWABU: Na'am, inaruhusiwa kwa mwanamke kutumia tembe zenye kuzuiya heidh katika wakati wa Hijjah kwa kuichelea heidh yake isimjie. Lakini jambo hilo ni baada ya kumtaka shauri Daktari atakae kumuhakikishia yakwamba afya yake haitoathirika. Vilevile, anaweza kufanya kama hivyo katika mwezi wa Ramadhaan ikiwa atapendelea kufunga na watu. [Hakuna haja ya wanawake kufikiya upeo huo. Huwenda hali hii ikazingatiwa kuwa ni aina fulani ya kupindukia mipaka. Hakuna uhakikisho wa kweli kuhusiana na athari za ki-afya za tembe kama hizo, kama tembe za upangaji wa mimba. Zaidi ya hayo, heidh ni jambo la asilia ambalo Allâh Amelija'alia kwa wanawake na haina haja ya kulikwepa hilo. Kwa hiyo, ni lazima lizingatiwe kuwa ni jambo bora kwa wanawake kujiepusha na tembe kama hizo kwani hawawezi kuwa na uhakika kuhusiana na madhara yake. Allâh ndiye Mjuzi zaidi.]

Kamati ya Wanavyuoni:

KUKATIKA KWA DAMU KATIKA WAKATI WA HEIDH:

SUALI: Mara nyengine hunitokea, katika wakati wa heidh yangu, yakwamba hupata damu kwa siku nne kisha mara husimama kutoka kwa siku tatu. Kisha katika siku ya saba, damu hunirudia, lakini haiwi ya nguvu kama ile iliyotangulia. Kisha hugeuka na kuwa rangi ya hudhurungi au kahawia (Brown) mpaka katika siku ya kumi na mbili. Natumai utaniongoza juu ya jambo la sawa katika suala hili.

JAWABU: Masiku ulioyoyataja, siku ya nne na siku ya sita, ni masiku ya heidh. Hufai kuswali wala kufunga katika masiku hayo. Haifai kwa mumeo kukuingilia katika siku hizo. Itakupasa ujitwahirishe (utekeleze Ghusl) baada ya siku nne kisha uswali na mumeo ataruhusiwa kuingiliana na wewe wakati huo baina ya siku nne na siku sita. Pia hakuna uharamu juu ya kufunga kwako. Ikiwa hayo yatatokea katika mwezi wa Ramadhaan, utawajibika kufunga. Na utakapotwahirika baada ya hizo siku sita, itakulazimu utekeleze Ghusl, uswali na ufunge kama ilivyo katika wakati wowote za kutwahirika. Hii ni kwa sababu ada ya kila mwezi inaweza kuongezeka na kupungua. Mara nyengine masiku yake hushikana pamoja na mara nyengine huwa mbalimbali. Twamuomba Allâh atuongoze sote katika yenye kumridhisha Yeye. Twamuomba atupe sisi, wewe na Waislamu wote ufahamu na msimamo kwenye Dini.

Sheikh Ibn Baaz.

MATONE YA DAMU BAADA YA KUTEKELEZA GHUSL:

SUALI: Nimegundua yakwamba mara nyengine baada ya kutekeleza Ghusl kutokana na ada yangu ya mwezi, baada ya kumaliza ada yangu ya kiwango cha muda wa kawaida, siku tano, nilitokwa na kiwango kidogo sana cha vitone vya damu. Na hii hutokea punde tu baada ya kutekeleza Ghusl. Kisha baadae, hakuna chochote kitokacho. Sasa sijui nifanyeje. Nifuate siku zangu tano za kawaida bila ya kujali yatokeayo baada ya hayo na niendelee kuswali na kufunga? Au niizingatie siku hiyo pia kuwa ni sehemu ya ada yangu nisiswali wala nisifunge katika wakati huo? Ukumbuke yakwamba mambo hayo hayanitokei kila mara isipokuwa hutokea katika kila ada mbili, tatu, au kama hivyo. Natumai utanifaidisha kuhusiana na suala hili.

JAWABU: Ikiwa kinachokutoka baada ya kujitwahirisha ni emma manjano au hudhurungi, haifai kuzingatiwa (kuwa ni heidh) na hukmu yake ni sawa na hukmu ya mikojo.Hatahivyo, ikiwa inaonyesha wazi kuwa ni damu, itazingatiwa kuwa ni katika sehemu ya heidh na utalazimika kurudia tena Ghusl kutokana na yaliyothubutu kutoka kwa Umm 'Atiyyah (رضي الله عنهما) Mmojawapo wa Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliyesema baada ya kutwahirika kutokana na heidh: *"Hatukuzingatia chepechepe ya manjano na hudhurungi kuwa na umuhimu wowote."*

Sheikh Ibn Baaz.